



Australian Government

Department of Health

Habari ya kufaa juu ya chanjo za COVID-19

Utoaji wa Chanjo za COVID-19

Chanjo za COVID-19 zinaendelea kupewa kwa watu nchini Australia.

Chanjo za COVID-19 zitakusaidia wewe, familia yako na jamii yako kuzuia ugonjwa wa COVID-19. Chanjo hizo ni bure kwa kila mtu nchini Australia, hata ikiwa wewe sio mraia au mkaazi wa kudumu wa Australia. Hawa wanajumuisha watu bila kadi ya Medicare, wageni wa nje, wanafunzi wa kimataifa, wafanyakazi wahamiaji na watafutaji wa usalama.

Huna haja kuwa na kadi ya Medicare ili kupata chanjo yako katika kliniki za chanjo za serikali. Utahitaji kadi ya Medicare kama unaenda kwa daktari wa familia.

Kuhusu chanjo za COVID-19

Chanjo huimarisha mfumo wako wa kinga kwa kufunza mwili wako kukumbuka haraka na kupambana na vijidudu fulani.

Ushahidi wa mapema unaonyesha kuwa chanjo za COVID-19 husaidia kupunguza kueneza kwa virusi hii.

Unaweza bado kupata kupata ugonjwa wa COVID-19 hata baada ya chanjo yako, lakini chanjo hii itakulinda kukuzuia kuwa mgonjwa sana. Tunahitaji chanjo ili kusaidia kukomesha janga, kupunguza idadi ya kesi, na kusimamisha virusi ili isibadilike.

Chanjo za COVID-19 za Australia zinafanya kazi kwa ufanisi sana kuzuia ugonjwa, watu kulazwa hospitali na vifo kutokana na ugonjwa wa COVID-19.

Wanasayansi wataendelea kukusanya ushahidi juu ya athari zinazoendelea kutoka chanjo.

Chanjo zote za COVID-19 nchini Australia huendelea kufuatiliwa kwa karibu kwa usalama.

Wewe unahitaji dozi mbili za chanjo ileile kwa kinga bora kudhidi ugonjwa wa COVID-19. Katika miadi yako ya kwanza, wafanyakazi watakuambia wanapoweka miadi kwa dozi yako ya pili.

Je, nawezaje kuweka nafasi kupata chanjo yangu ya COVID-19?

Ili kujua zamu yako wakati inapokuwa zamu yako ili kupata chanjo za COVID-19, unaweza kutumia Kikagua cha Kustahiki (Eligibility Checker) kwa www.health.gov.au

Mara unapokamilisha Kikagua cha Kustahiki utaona orodha ya maeneo unayoweza kuwasiliana ili kuweka nafasi kupata chanjo yako karibu kwako.

Baadhi ya majimbo na wilaya zitabadilika ustahiki wao kutegemea na hali yao ya ugonjwa wa COVID-19 na utoaji wa chanjo na matumizi ya chanjo. Uendelea kujua hali ya kisasa na habari kutoka idara ya afya ya eneo lako ili kuona kama imebadilisha mahitaji yao ya ustahiki.

Maelezo zaidi juu ya ugonjwa wa COVID-19 na chanjo za COVID-19

Ni muhimu kuendelea kuwa na taarifa kupitia vyanzo vya rasmi. Kwa maelezo juu ya utoaji wa chanjo za COVID-19 nchini Australia, au habari zaidi kuhusu jinsi ya kuweka nafasi kwa chanjo yako ya COVID-19, tembelea kwa [health.gov.au](https://www.health.gov.au) au pigia simu kwa Simu ya Msaada wa Kitaifa ya Virusi vya Korona kwenye 1800 020 080. Kwa huduma za utafsiri na ukalimani, pigia simu kwenye 131 450.